GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA


MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **248** Sha'ban-Ramadhan **1446** AH Februari– **2025** Tabligh **1404** HS BEI TSH 800/=

UFUNUO WA HADHRAT SAYYIDNA AHMADas

KUHUSIANA NA MWANA ALIYEAHIDIWA[RA]



Hazrat Mirza Ghulam Ahmad of Qadian
The Promised Messiah & Mahdi
(peace be upon him)

"Ninakupa Ishara ya Rehema Yangu kwa kuyajibu maombi yako. Nimeyasikia maombi yako na nimekirimu dua zako kwa ukubali Wangu kwa njia ya rehema Yangu na nimeibariki safari yako hii. Ishara ya Qudra na uwezo, ukarimu, ukaribu Nami inatolewa kwako. Ishara ya rehema na ihsani inaletwa kwako na unapewa ufunguo wa ufaulu na ushindi. Amani iko juu yako, ewe mshindi. Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu ili kwamba wale wanaotamani uzima waokolewe kutoka mkamato wa mauti na wale waliolala makaburini wafufuliwe na ili kwamba utukufu wa Islamu na heshima ya neno la Mungu Mwenye Enzi idhihirike mbele ya watu na ili kwamba ukweli uwasili pamoja na Baraka zake zote na uongo utoweke pamoja na nuksi zake zote, na ili kwamba watu waweze kuelewa ya kwamba Mimi ni Mwenye Nguvu, Ninafanya Nipendavyo. Na ili kwamba wawe na yakini ya kuwa Mimi Niko pamoja nawe, na ili kwamba wale wasio mwamini Mungu Mwenye Enzi na wanakana na kukataa dini Yake na kitabu Chake na Mjumbe Wake Mtakatifu, Muhammad Mteule (saw) wakabiliane na ishara iliyo wazi na ili njia ya wakosefu iweze kubainika.

Basi furahi ya kwamba utajaaliwa mtoto mwanamume mtakatifu na mzuri, utampokea kijana mwana ambaye atakuwa ni mbegu yako na kizazi chako. Kijana mzuri na mtakatifu atakuja kama mgeni wako. Jina lake ni Emmanuel na Bashir. Amejazwa roho takatifu, na ameepukana na uchafu wote. Ni nuru ya Allah. Amebarikiwa yule ajaye kutoka mbinguni. Atafuatana na rehema ambayo itawasili pamoja naye. Atahusishwa na utukufu, ukuu na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya Baraka za Roho ya kweli. Yeye ni Neno la Allah kwani ukarimu na heshima ya Allah imemtuma na Neno la Utukufu. Atakuwa na akili sana mno na ufahamu na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa elimu ya nje na ndani. Atawafanya watatu kuwa wane (hii maana yake haikubainishwa). Ni Jumatatu, Jumatatu iliyobarikiwa. Mwana wa kiume, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, mtukufu.

مظهرالاول والاخرمظهرالحق والعلاء كان الله نزل من السماء

Mdhihirishaji wa Aliye ni wa Mwanzo na Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na wa Juu; kana kwamba Allah Ameshuka kutoka mbinguni. Kufika kwake kutabarikiwa sana sana na atakuwa sababu ya kudhihirika kwa Jalali ya Uungu. Nuru inakuja, nuru hasa, nuru iliyosingwa na Mwenyezi Mungu uturi wa mapenzi Yake.Tutampulizia roho yetu atahifadhiwa chini ya Kivuli cha Mwenyezi Mungu. Atakuwa upesi upesi katika umbo na atakuwa sababu ya kukombolewa wale waliomo utumwani. Atajulikana mpaka pembe za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake. Ndipo atachukuliwa juu mbinguni kwenda mahali alipotayarishiwa.

و كان امرا مقضيا

Na jambo hili limekwisha katwa tayari"



Hazrat Mirza Basheer-ud-Din Mahmood Ahmad Khalifatul Masih II.



Minarat ul Masih Qadian

Maneno ya Bishara kumhusu Mwana Aliyeahidiwa[as] UK. 03

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SULTANI WA KALAMU

Utamaduni wa magharibi unaoamini katika itikadi ya bila utafiti hakuna haki ya kuzungumza kwa masikitiko makubwa itikadi hii wameiweka kapuni wakati wanaandika juu ya historia ya mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Ni aibu na fedheha katika ulimwengu wa wasomi, waandishi maarufu wa magharibi walishika kalamu na kila ubaya unaoweza fikiri alipakwa Mtukufu Mtume Muhammad saw.

Masingizio yote hayakuwa na msingi na sisi waswahili tunafahamu, akutukanaye hakuchagulii tusi. Katika hali hiyo ya kujiamini na huku wakisaidiwa na serikali za kikoloni zilizokuwa zinatawala wakati huo.

Matangazo yalitoka kuwa miaka michache imebaki na Islam itabaki tu katika nyumba za Makumbusho na Msalaba utatawala dunia. Kiwango cha wanaoingia katika ukristo ikawa inaongezeka siku hadi siku.

Ni wakati huo wa maumivu makubwa Allah alipomuinua Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] ambaye alivunja misalaba, akaonesha udhaifu wa ukristo na kudhihirisha ubora wa dini ya Islam. Sultan wa kalamu aliendesha jihadi ya kalamu kwa kuandika vitabu zaidi ya 80. Matokeo yake vitabu hivi vimeleta mapinduzi makubwa na wasomi wakubwa wakubwa wameathirika sana na kutoa maoni. Tutatizama wasomi hao wachache ili kumaizi ni kwa kiasi gani kalamu ya Masih Aliyeahidiwa ilivyoleta Mapinduzi makubwa ya fikra kuhusu Mtukufu Mtume Muhammad[saw].

Profesa Laura Veccia Mangheri aliacha njia ya wenzake yeye akajikita katika kutafuta ukweli. Alijitahidi kusoma kila kitabu kuhusu Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Katika kusoma vitabu akakutana na vitabu vya Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Maandiko yenye usafi wa hoja yalimvutia sana na Profesa huyu wa kiarabu na utamaduni wa kiislam chuo cha Naples akashika kalamu na kupatia dunia kitabu kinachoheshimiwa sana na wasomi.

Kitabu hicho ni "Interpretation of Islam". Katika kitabu hicho ukurasa wa 8, kuhusu Mtukufu Mtume Muhammad[saw] anaandika "Muhammad kama muhubiri wa dini ya Mwenyezi Mungu alikuwa mpole na mwenye huruma hata kwa wale waliokuwa maadui zake binafsi. Katika hulka yake kulikuwa kumejaa haki na uadilifu".

Mwana historia ambaye amefanya utafiti wa kina katika nchi za kiislam Lamartine, katika kitabu chake ambacho kila mwana historia wa Islam anacho katika maktaba "History of Turkey"-uk 76 anaandika kuhusu Mtukufu Mtume Muhammad[saw], "mwanafalsafa, bingwa wa hotuba, mtungaji wa sheria, mahiri wa fikra. Mwanzilishi wa dola moja ya kiislamu. Huyu ndiye aliyekuwa Muhammad. Ukichukua vipimo vyote vinavyopima umaarufu wa mtu, tunaweza kujiuliza, kuna wa kumzidi"? Msomi I Der Menghem katika The "Life of Mohamed" ukarasa wa 171 anatueleza, "Muhammad alidhihiri
wakati wa giza totoro ambako historia haijawahi kushuhudia. Wakati ustaarabu kutoka Merovingian Gaul hadi India ulikuwa katika maangamio makubwa. Walikuwa katika hali ya mgonjwa mahututi-bila shaka mgonjwa alipewa tiba na Mtukufu Mtume Muhammad[saw]".

Profesa W. Mongomery Wati ni maarufu sana na ameandika vitabu vingi lakini vilivyompatia jina ni "Muhammad at Mecca" na "Muhammad at Medina". Ukivisoma utaelewa kwamba msomi huyu alikwenda maili moja zaidi katika kutafuta maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Katika kitabu chake Muhammad at Medina uk. 336 anatukumbusha mtu anapozidi kutafakari juu ya historia ya Muhammad na Islam ya mwanzoni hapo ndipo anapozidi kushangaa kuhusu mafanikio yake. Hali halisi ilimpatia fursa ambayo ni wachache wanaoipata. Lakini bwana huyu alikuwa sawa na wakati. Na kama isingekuwa hidaya aliyopewa ya yule anayeona mbali, kiongozi shupavu, imani yake katika Mwenyezi Mungu na imani yake thabiti kwamba Mwenyezi Mungu Amemtuma, ukurasa muhimu katika historia ya binadamu usingeandikwa".

Huo ndio upanga wa kalamu aliuleta Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ambao unakata kuwili upande mmoja unatoa hekima na upande mwingine unatoa utakaso. Huu ni wakati wa binadamu wote kuvisoma vitabu vya Nabii wa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye ametumwa kutibu maradhi yanayotusibu. Tusifanye ukorofi. Tunywe dawa. Tusiwe na ukorofi wa yule mshairi aliyesema, sili nisichotamani sili ingawa ni dawa. Ni mtu wa kusikitikia anayekataa dawa.

Tunamshukuru Allah ulimwengu wa kiswahili unavyo vitabu vingi vya Masih Aliyeahidiwa (as) vilivyotafsiriwa katika lugha yetu adhimu. Tusipoteze wakati dawa imekwisha patikana tuitumie.



QUR'AN TUKUFU

9. Na ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao. *Al-Mu'Minuun 23:09*

وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمَانَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ۝٩



NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar r.a. ya kwamba Mtume[saw]. alisema: Kila mmoja wenu ni mchungaji na kila mmoja wenu ataulizwa kuhusu raia wake. Amiri ni mchungaji. Na mtu ni mchungaji wa watu wa nyumbani mwake. Na mwanamke ni mchungaji wa nyumba ya mumewe na watoto wake. Basi kila mmoja ni mchungaji na kila mmoja ataulizwa kuhusu raia wake. (Bukhari)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

Moyo wangu unakuwa hautulii kufikiria kwamba watu hawa ambao wana muelekeo wa njia iliyo nyooka hawajiletei madhara peke yao kutokana na maovu yao wenyewe, badala yake, huwapa wengine fursa ya kuucheka Uislamu pia. Ni kwa sababu hii kwamba katika sensa iliyotangulia, Bw Ibbetson ameandika mengi juu ya Waislamu. Katika hili, nataka kubainisha kwamba Waislamu wanajiita Waislamu lakini wanahusishwa na vitendo vya haramu na haramu ambavyo sio tu vinawatia shaka, bali pia Uislamu. Kwa ufupi, tengeneza tabia na mwenendo wako kwa namna ambayo hata makafiri (ambao kwa hakika wanataka kuukosoa Uislamu) wasiweze kupata kosa kwako.

Mwisho...

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

SALUM DADI MTAMILA KATUTOKA

Na Mwana Historia wetu

Saa kumi na mbili asubuhi juu ya alama, simu inaita kutizama ni Bwana Musa Rashid Nyumba napokea.

Assalam Aleikum, naitikia Waalekhum Salaam inna lillah wa inna ilayhi raajiun, Bwana Salum Dadi Mtamila ametutoka usiku wa jana tarehe 25/12/2024 naitikia inna lillah wa inna ilayhi raajiun.

Kumbukumbu yangu ya kwanza juu ya Mtamila ni mahaba na jazba yake ya kufikisha ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as), kwa hili alikuwa mstari wa mbele na alikwenda kufanya mahubiri katika sehemu nyingi za nchi. Hakuchoka hata kidogo kufanya kazi adhim ya kutanguliza dini mbele ya kila kitu. Bwana Ramadhani Athumani Shamte ndiye aliyemhubiria kwa kumpa vitabu vya Jamati alivyovipitia kwa shauku kubwa sana. Huko nyuma alikuwa amepata elimu nzuri ya dini katika chuo cha Maalim Abubakar Kinguyu ambako alisoma na Sheikh Bakri Abedi Kaluta. Hivyo alivisoma kwa makini na akaamua kujiunga.

Sifa yake kubwa ambayo sasa inatakiwa ihimizwe zaidi ni usomaji wa vitabu, katika hili hakuwa tayari kupoteza muda. Alivisoma kwa makini na hili lilidhihirika katika mahubiri yake yaliyoonesha elimu pana ya dini ya Islam. Salum Dadi Mtamila alikuwa na mfungamano mkubwa na msikiti. Mara kwa mara alikuwa msikitini akitoa uzoefu wake katika mahubiri. Kwa kazi za Jamati Salum Dadi Mtamila hakuwa nyuma. Kila ilipotakiwa huduma alijitokeza na kushiriki, itakumbukwa ya kuwa aliwahi kuwa katibu wa Rishta Nata Taifa na aliweza kufanya kazi nzuri.

Salum Dadi Mtamila alikuwa nadhifu na alipenda kuvaa vizuri na mara kwa mara alisema mwislamu anatakiwa kuwa nadhifu. Kila Ahmadiyya unayemuona ukifanya uchunguzi utagundua kuna somo unaweza kupata katika maisha yake. Mtamila ametuachia yafuatayo:-

a) kuwa tayari kusoma chochote bila kujiwekea mipaka. Alipokea vitabu vya Jamati na kumuongoza kwenye njia iliyonyooka.

b) Utamaduni wa kusoma aliuheshimu sana na kila kitabu kipya kilipotoka alikuwa miongoni mwa watu wa kwanza wa kusoma kitabu hicho.

c) Mahubiri ilikuwa mkate wake wa kila siku, nasi tuufanye uwe mkate wetu wa kila siku in shaa Allah.

Tunamuomba Allah Azipokee juhudi zake na kumsamehe makosa yake kwani Allah ni Ghafuru Rahim.

Maneno ya Bishara kumhusu Mwana Aliyeahidiwa[as]

A"mebarikiwa yule ajaye kutokambinguni.Atafuatana na rehema ambayo itashuka Pamoja naye. Atahusishwa na utukufu, ukuu, na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya baraka za Roho ya kweli. Yeye ni neno la Allah kwani ukarimu na heshima ya Allah imemtuma na Neno la Utukufu. Atakuwa na akili sana mno na ufahamu na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa na elimu ya nje na ndani. Atawafanya watatu kuwa wanne.(hii maana yake haikubainishwa).

Ni Jumatatu. Jumatatu ilyobarikiwa. Mwana wa kiume, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, mtukufu, mdhihirishaji wa Aliye ni wa Mwanzo na Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na wa Juu.

Kana kwamba Allah ameshuka toka mbinguni. Kufika kwake kutabarikiwa sana sana na kutakuwa sababu ya kudhihirika kwa jalali ya Uungu. Nuru inakuja, nuru hasa , nuru iliyosingwa na Mwenyezi Mungu uturi wa mapenzi yake. Tutampulizia roho Yetu atahifadhiwa chini ya kivuli cha Mwenyezi Mungu. Atakuwa upesi upesi katika umbo na atakuwa sababu ya kukombolewa wale walio utumwani. Atajulikana mpaka pembe za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake. Ndipo atachukuliwa juu mbinguni kwenda mahali alipotayarishwa na jambo hili limekwisha katwa."

{Tangazo la tarehe 200 Februari, 1886 }.

Kisha Seyyedna Ahmad a.s. aliandika akinukuu funuo kwamba:

"Rehema itafika pamoja na kuja kwake. Yeye ni nuru na ni mabruk na mtakatifu na yu miongoni mwa watawa. Ataeneza baraka na atawalisha watu chakula safi na atakuwa mwenye kuinusuru dini…. Atakuwa mmoja kati ya ishara zangu na atakuwa Beramu ya misaada yangu ili kwamba wale wanaokukadhibisha wajue ya kuwa mimi niko pamoja nawe kwa njia ya rehema yangu iliyodhihirika……..

Atakuwa na ufahamu na akili na atakuwa mwenye kupendeza. Moyo wake utajazwa elimu, batini yake itakuwa na upole na kifua chake kitajazwa utulivu. Atajaaliwa na roho ya Umasihi na atabarikiwa na roho mwaminifu. Jumatatu,Jumatatu iliyobarikiwa,Roho za watu wenye baraka zitafika kwako"(Ainae kamalate Islam uk 577-578).

JALSA SALANA QADIAN KIINI CHA SAFARI YA KIROHO

Kutoka uk. 12

Ahmadiyya.

Makala haya kimsingi yanaelezea upekee wa Jalsa Salana Qadian. Mwanzoni mwa makala haya tumejizatiti kuhusu heshima kubwa waliyonayo waahmadiyya kwa mji ambao sasa una lakabu ya Qadian Darul-amani. Historia katika makala hii imeelezwa ili kuonesha athari ya Qadian kwa waahmadiyya, umma wa kiislamu na dini zote duniani kwa ujumla.

Qadian ni dhihirisho la Allah kuhusu kusimamisha utume na nidhamu ya ukhalifa katika umati bora wa mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Jalsa Salana Qadian ni picha iliyokamilika ya Jalsa ya kimataifa inayowaleta pamoja waahmadiyya kutoka pembe zote za dunia. Tutaeleza ingawaje kwa muhtasari sababu zinazowasukuma binadamu kila pembe kuhudhuria Jalsa Salana Qadian.

Itaendelea in shaa-Allah toleo lijalo.

TANGAZO

UONGOZI WA LAJNA IMAILLAH TANZANIA UNAWATANGAZIA LAJNA NA NASRAT WOTE NCHINI KUWA IJTIMAI YA LAJNA IMAILLAH YA MWAKA 2025 ITAFANYIKA TAREHE 20,21 & 22 YA MWEZI JUNI KATIKA ENEO LETU LA KITONGA JIJINI DAR ES SALAAM.

KILA MWANATANZIMU ANAHIMIZWA KUMALIZA MCHANGO WAKE WA IJTMAI NA KUWEKA NIA YA DHATI YA KUHUDHURIA IJTMAI HIYO PAMOJA NA KUJIANDAA KUSHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA KIELIMU NA MICHEZO.

PIA WANATANZIMU WANAKUMBUSHWA KUSHIRIKI SHINDANO LA INSHA PAMOJA NA LILE LA QURAN KWA NJIA YA KUJIREKODI AMBAPO MWISHO WA KUTUMA INSHA NA AUDIO HIZO ZA QURAN KWA WASHIRIKI WOTE NI TAREHE 29/02/2025.

PIA WAJUMBE WOTE WA SHURA KUTOKA MATAWI MBALIMBALI NCHINI WANAKUMBUSHWA KUJIANDAA NA SHURA YA KITAIFA ITAKAYOFANYIKA SIKU YA JUMAPILI YA MWEZI JUNI.

WASALAAM.

Jalsa Salana ya Mkoa, Pwani yafana

Na. Maliki Mbawala
Kibiti, Pwani

Kwa fadhila na msaada wa Allah Jumuiya ya WaisalamuAhmadiyya mkoa wa Pwani imeweza kufanya Jalsa salana katika mkoa wa Pwaniwilaya ya Rufuji, mkutano huo ulikua siku ya jumamosi tarehe 04/01/2025 na ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa chuo cha ufundi FDC-IKWIRIRI College kata ya Ikwiriri. Kwa ujumla tulipata mafanikio makubwa katika Jalsa salana hiyo katika Nyanja mbalimbali.

MAHUDHURIO

Mkutano wetu ulihudhuriwa na wanajamaati wa matawi yote ya mkoa wa Pwani pamoja na mikao ya jirani. Idadi ya waliohudhuria ni 377 wanaume ni 198 na wanawake ni 179 wageni kutoka nje ya mkoa wa Pwani ni 36 wageni ambao sio Wahmadiyya jumla walikua 46 wanawake ni 21 wanaume 25, kwa muktadha huo idadi halisi ya mahudhurio ya wanajamaat katika mkoa wa Pwani ni 295 haya ni mafanikio makubwa kwani tumevuka lengo ambalo lilikua ni wanajamaat 250 Alhamdulilahi. Kiongozi wetu mpendwa wa kitaifa Amir na mbashiri mkuu Sheikh Khawaja Muzaffar alihudhuria na alipata kuongoza shughuli mbalimbali Mkuu wa wilaya ya Rufiji alialikwa kama mgeni rasmi lakini alimtuma muwakilishi wake MheshimiwaAlly Ndungutu ambaye ni Diwani wa kata ya ikwiriri na naibu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Rufiji.

RATIBA YA JALSA SALANA

Matukio ambayo yalipangwa katika ratiba yalikwenda sawa na mpangilio usomaji wa Quran tukufu uilsomwa na Bw. Ramadhani Zaharani, usomaji wa shairi Bw. Abubakari Y. Kambaulaya, Raisi wa Mkoa wa Jamaat alitoa hutuba fupi ya kukaribisha wageni na utambulisho katika mkutano huo, kisha hutuba ya kwanza ya jalsa salana ilitolewa na Maulana Sheikh Abdurahmani Ame iliyojikita katika wajibu wa mume na mke katika maisha ya ndoa, hutuba ya pili ilitolewa na Maulna Sheikh Nadeem Ahmed ilibainisha nidhamu ya ukhalifa :ni jambo gani tunaweza kulifanya kuimarisha nidhamu ya ukhalifa, shairi la pili lilisomwa na ndugu Kasimu Muhamedi Mlekeni kisha hutuba na salamu mgeni rasmi iliwasilishwa na Diwani Mheshimiwa Ally Ndungutu ambaye pia ni naibu Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Rufiji ambaye alionesha hisia zake kuwa jamaati Ahmadiyya ni taasisi ya kipekee ya kidini ambayo taratibu zake zimekuwa na nidhamu kwani hatuoni migogoro ikipelekwa hata bakwata ama serikalini hii inaonyesha mnauongozi imara alipatiwa zawadi mbalimbali ya vitabu na majarida ya jamaati. Hutuba ya mwisho ilikuani ya Amir Sahib ambayo ilijielekeza katika Nyanja mbalilmbali juu ya wana jamaati kutimiza wajibu wao katika kuitumikia islamu na jamaat na aliwahimiza wazazi kuwatoa vijana wao katika njia ya Mwenyezi Mungu kwenda Jamia kusoma masomo ya dini na kuitumikia dini. Kisha Amir sahib akaongoza maombi ya kufunga Jalsa Salana na akasalisa sala ya Adhuhuri na Alasiri.

CHAKULA

Baada ya sala ya adhuhuri na alasiri ilifuata ratiba ya chakula, chakula walipatiwa wageni wote waliohudhuria pamoja na maji katika mkutano huo. Mwishoni Amir Sahib aliongoza kikao kifupi cha wajumbe wa majlis amila zote za matawi katika kikao hicho Amir Sahib alisisitiza juu ya majlis za matawi kufanya vikao vyake katika kila mwezi na kujadili changamoto zao na kisha zile ambazo zimewashinda kuzituma makao makuu.

KUCHANGIA DAMU

Katika Jalsa Salana hiyo Khudaamul Amadiyya Mkoa wa Pwani waliandaa zoezi la kuchangia damu na katika zoezi hilo Unit 18 za damu zilipatikana. Katika mchanganuo Lajna 7, Anasruulah 2 na Khuddam 9 ndio walio jitolea damu kati siku hiyo. Watu wa damu salama walisifu namna tukiolilivyo pangwa na utaratibu mzuri na walifurahi sana kwani walitoa sifa za kipekee kuwa hawajawahi kuona mkutano wenye utaratibu mzuri kama huu wa Ahamadiyya.

VYOMBO VYA HABARI (RUFIJI- FM)

Taarifa za Jalsa Salana zilirushwa na redio ya Rufiji FM katika kipindi cha MIZANI YA ASUBUHI
inakadiriwa kuwa zaidi ya watu 750,000 walipata habari za Jalsa salana kwani redio hiyo inasikika katika maeneo ya Kibiti ,Rufiji na Kisiwa cha Mafia.

TAARIFA YA ZIARA YA AMIR NA MBASHIRI MKUU KATIKA MKOA WA PWANI



Kwa fadhiliza Allah tulimpokea Amir na mbashiri mkuu katika mkoa wa Pwani mnamo tarehe 04/01/2025 saa 4 asubuhi akiwa na msafara wake, Mnamo tarehe 05/01/2025 alianza ziara yake katika Matawi 4 nayo ni Nambanje ,Mkongo , Kibiti na Bungu

MAHUDHURIO YA WANAJAMAAT

- Nambanje 45.
- Mkongo 47.
- Kibiti 42.
- Bungu 37.

Kwa mwendelezo wa Makala hii piga simu au WhatsApp +255 658 971 662

TUSIYOYAJUA KUHUSU QUR'AN TUKUFU KUHIFADHIWA KWAKE

Na Sheikh Abid Mahmood Bhati
Jamia, Morogoro



Kuenea kwa haraka kwa elimu ya Qur'an Tukufu kwa njia hii kunaweza kuelezwa ni kutokana na tukio; la Amri Ibn Salamah mtoto mwenye umri wa miaka saba. Alikuwa akiishi kwenye ukingo wa chemchem ambapo wasafiri walikuwa wakipumzika kwa muda. Alikuwa bado kusilimu lakini alikuwa akisikiliza kwa wapita njia wakisoma Qur'an Tukufu na alihifadhi kiasi kikubwa cha Qur'an Tukufu kabla ya kujiunga na uislam. {Sahihi Bukhari}.

UANDISHI WA QUR'AN TUKUFU KATIKA ZAMA ZA MTUME MUHAMMAD^{saw}

Ijapokuwa kuhifadhiwa kwa Qur'an Tukufu kulifanywa zaidi kwenye kumbukumbu za maswahaba. Mtume Muhammad (s.a.w) alifanya mpango mahususi ili ihifadhiwe vilevile. Njia iliyotumika kufikia lengo hilo imeelezwa na Sayyidna Zayd bin Thabit (r.a) kwenye hadithi hii kwamba'' nilikuwa nikiandika wahyi kwa ajili ya Mtume wahyi ulipomshukia; alihisi joto kali na matone na jasho yakibubujika mwilini mwake kama lulu.hali hii ilipokoma nilikuwa nikichukua mfupa wa bega au kipande cha kitu kingine na aliendelea kunisomea imla nikiandika nilipomaliza kuandika uzito wa maandiko ulinipa hisia ya kuwa mguu wangu ungevunjika na nisingeweza kutembea tena hata hivyo nilipomaliza kuandika aliniambia soma na nilimsomea, kama palikuwa na makosa aliisahihisha na kisha iliwasilishwa mbele za watu {Tabaran alawsat majma az-zaid}.

Sayyidna Othman^{ra} alieleza kuwa ilikuwa tabia ya Mtume Muhammad (s.a.w) ukiacha kutoa faida ya wahyi alimwelekeza mwandishi kuandika aya Fulani na sura Fulani kwa hiyo ilikuwa ikiandikwa kwa utaratibu huo.

Kwa hiyo wakati wa Mtume Muhammad (s.a.w) nakala moja ya Qur'an Tukufu ilijumuisha yale aliyoyasimamia kuandikwa japokuwa hayakuwa kwenye hali ya kitabu bali kwenye vipande tofauti pamoja na hivyo baadhi ya maswahaba waliandika aya za Qur'an Tukufu kwa ajili ya kumbukumbu zao hali hii ilikuwa toka mwanzo wa uislam kama ilivyoshuhudiwa na Hadhrat Fatma bint Al Khattab (r.a) dada yake Sayyidna Umar (r.a) na mume wa Zayd bin Zaid aliyesilimu kabla ya Sayyidna Umar (r.a) na aliposikia anaingia ndani ya nyumba yao kwa mshangao alikuta vipande vilivyoandikwa aya za sura Twaha vilivyoandikwa na Sayyidna khattab bin arrat r.a ambaye alikuwa akiwafundisha {Sunan dar qutn juz 1 uk 223}

Zaidi ya hayo kuna hadithi zinazoonyesha kuwa masahaba walikuwa na nakala zilizoandikwa Qur'an Tukufu kamili au pungufu kwa mfano bukhari alimnukuu Ibn Umar r.a akisema ''Mtume Mtukufu amekataza kuchukua Qur'an kwenye nchi za maadui (Bukhari kitabu jihad juz 1 uk 419-420)

Pia kuna hadithi kwenye Mujam tabarani ya kwamba Mtume Muhammad^{saw} alisema iwapo mtu yeyote atasoma Qur'an bila kuangalia maandishi malipo yake ni mara elfu moja na akisoma kwenye maandishi malipo yake ni mara elfu mbili [az-zawaaid juz 7uk 165]

NJIA ZILIZOTUMIWA KULINDA NA KUHIFADHI QUR'AN TUKUFU

Mara tu wahyi ulipopokelewa na Mtume Muhammad (s.a.w) huo ulirekodiwa kimaandishi moja kwa moja kutoka kinywa chake wanafahamika watu kadhaa kuwa ndio waliotumiwa na Mtume Muhammad (s.a.w) kwa madhumuni haya, miongoni mwao majina ya hawa kumi na watano majina yao yametajwa katika hadithi {fathul bari uk 19]

(1)Hadharat Zaid bin Thabit r.a
(2)Hadharat Ubayy bin kaab r.a
(3)Hadharat Abdullah bin saad bin sarh r.a
(4)Hadhrat Zubair bin Al awwam
(5)Hadhrat Khalid bin said bin al 'aas
(6)Hadhrat Aban bin Said bin Al-'aas
(7)Hadhrat Handhala bin Ar-rabii al-asadii r.a
(8)Hadhrat Muaiqib bin abii Fatima r.a
(9)Hadhrat Abdullah bin Arqam Az-zuhr r.a
(10)Hadhrat Shurahbil bin hasana r.a
(11)Hadhrat Abdullah bin Rawaha r.a
(12)Hadhrat Abuu bakar r.a
(13)Hadhrat Umar r.a
(14)Hadhrat Uthman r.a
(15)Hadhrat Alli r.a

Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w) alikuwa daima akisisitiza sana kuijua Qur'an Tukufu kwa moyo kiasi hiki kwamba Mtume Muhammad (s.a.w) alisema kuwa'' kama mtu akiijua Qur'an kwa moyo basi ataepushwa na adhabu ya jehanamu''. Mwenyezi Mungu alimjaalia Mtume Muhammad (s.a.w) masahaba ambao daima walijichumia wema kwa kila njia hivi kwamba alipotoa tangazo hili idadi kubwa miongoni mwao walianza kuhifadhi Qur'an Tukufu kwa moyo wakiwemo wale ambao ndimi zao hazikuwa fasaha sana na hawakuwa wenye elimu yoyote.

Imam Ahmad bin hambal amesimulia kufuatia hadhrat Abdullah bin Umar (r.a) ya kuwa mtu mmoja alimjia Mtume s.a.w na akamwambia Ewe Mtume wa Allah mimi naijua Qur'an Tukufu kwa moyo lakini akili yangu haifahamu vizuri maana zake. Hii inaonyesha kwamba haikuwa tu watu wenye elimu bali hata watu wa kawaida walikuwa na mazoea ya kuhifadhi Qur'an Tukufu kwa moyo.

Hadithi nyingine iliyosimuliwa na Hadhrat Ahmad bin Hambal kufuatia huyohuyo yaani Hadhrat Abdullah bin Umar anasema kwamba alimletea Mtume Muhammad^{saw} mwanawe na akasema Ewe Mtume wa Allah huyu mwanangu hushinda akisoma Qur'an Tukufu mchana kutwa na kulala usiku mzima Mtume Muhammad^{saw} akatamka akisema sasa pana lipi la kukutia wasiwasi mwanao hushinda akimkumbuka Allah badala ya kuleta udhia wowote yeye hujilalia. Kisa hiki chaonyesha kwamba hata wale watu wa kawaida walioishi mbali na Mtume Muhammad^{saw} walikuwa wameanza desturi ya kuhifadhi Qur'an Tukufu kwa moyo.

WAKUFUNZI WA QUR'AN TUKUFU

Kadri shauku ya watu ya kuhifadhi Qur'an Tukufu kwa moyo ilivyoongezeka Mtume Muhammad^{saw} aliteua wakufunzi wakuu wanne wa Qur'an Tukufu ambao walikuwa wakikariri chini ya usimamizi wa Mtume Muhammad^{saw} na kisha kuwafunza watu wengine kuhifadhi kwa moyo hawa wanne nao wakawafundisha watu kadhaa wengine ambao nao wakawa wenye kuifundisha Qur'ani Tukufu hao wanne walikuwa ni,

(1).Hadhrat Abdullah bin Masuud
(2).Hadhrat Salim Maula bin Hudhaifa
(3).Hadhrat Muadh bin Jabal
(4) Hadhrat Ubayy bin Kaab

Hawa wawili wa kwanza walikuwa ni watu wa Makka waliokuwa wamehamia Madina na hao wawili wa mwisho walikuwa ni maansar Hadhrat Abdullah bin masuud na Hadhrat Salim alikuwa ni mtumwa aliyeachiwa huru. Hadhrat Muadh na Hadhrat Ubayy walikuwa ni viongozi wa Madina kwahiyo Mtume Muhammad^{saw} alichagua wakufunzi wa Qur'an Tukufu kutoka miongoni mwa wenyeji mbalimbali ili asije mtu yeyote akapata shida kuwaendea na kujifunza kutoka kwao. Mtume Muhammad^{saw} alikuwa akisema wale miongoni mwenu wanaotaka kujifunza Qur'an Tukufu basi wakajifunze kwa Hadhrat Abdullah bin Masuud, Salim Maula bin Hudhaifa au Ubayy bin Ka'ab {Muslim}.

Inasimuliwa kwamba safari moja Hadhrat Abdullah bin Masuud alikuwa akiisoma Qur'an Tukufu hapo Hadhrat Umar ra alishauri kwamba neno Fulani litamkwe ipasavyo. Hadharat Abdullah bin masuud akalamika akisema kwamba yeye alikuwa amefundishwa na Mtume Muhammad (s.a.w) kulitamka neno lile lile alivyokuwa amelitamka Hadharat Umar (r.a) akampeleka kwa Mtume Muhammad^{saw} na kunung'unika ya kuwa Yule mwenziwe hakuisoma Qur'an Tukufu vilivyo, Mtume Muhammad^{saw} akatamka Hadharat Abdullah bin masuud (r.a) aisome ile sehemu iliyozusha maoni yanayotofautiana na alipoisoma Mtume Muhammad^{saw} akasema barabara kabisa, hapo Hadharat Umar (r.a) akasema kwamba nilikuwa nimefundishwa nawe kulitamka neno lile kivingine Mtume Muhammad^{saw} akamwambia aisome aya hiyo na alipofanya hivyo akamwambia na hivyo navyo ni barabara kabisa.

Kisa hiki chaonesha kwamba

Ukurasa wa 08

Bustani ya Washairi

TUNGA KWA ZILE KHABARI-ZIOKOAZO INSAFU

Ninajua Ashirafu, tungo zimekuathiri
Wasoma kimsahafu, vizuri wazikariri
Wala huna takhlifu, unapotunga shairi
Tunga kwa zile khabari, ziokoazo insafu

Waila nakuarifu, unapotunga shairi
Sheria usikhalifu, vina viende sanjari
Mizani siwe pungufu, ukamilishe urari
Tunga kwa zile khabari, ziokoazo insafu

Liwe kikuba wasifu, lisomwapo liwandari
Na humo ndani washufu, mkadi uso dosari
Wanukuu insafu, kama kamusi ya zari
Tunga kwa zile khabari, ziokoazo insafu

Tunga lugha usanifu, nogeza lugha vizuri
Useze ya unyoofu, uwaonye makafiri
Wape ya uchangamfu, waumini wa Qahari
Tunga kwa zile khabari, ziokoazo insafu

Kama tasimama safu, hivi kwenye mstari
Ukabaki mwangalifu, zako takuwa Bohari
Hazitakuwa pungufu, zitakuwa ni johari
Tunga kwa zile khabari, ziokoazo insafu

Al-Ustadh Mhenga
Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile Mbagala Rangitatu
Dar es Salaam

Litimize lengo lake
Alhamdu lillah, sifa wakushukuriwa
Wewe pekee Lillah,njia wakupambanuwa
Metuokoa wallah, kizani umetutowa
Litimize lengo lake, babu yangu abdullah

Moja nanenane nne, kundini aliingiya
Ahamadi aungane, akawa ahmadiya
Mkono akashikane, sheMaliki rafikiya
Litimize lengo lake, babu yangu abdullah

Jitahidi livoweza, ujumbe kuueneza
Marafiki naowenza, hakuacha waeleza
Mahubiri kwake kwanza, vidole hakuviwaza
Litimize lengo lake, babu yangu abdullah

Hajaacha jisomea, naumuri umekwenda
Tahajudi jiswalia, anadumu kwakupenda
Khuluka hazijapoa, japo siku zimekwenda
Litimize lengo lake, babu yangu abdullah

Tunakushukuru mungu, kwababu kumuongoza
Metuepusha viwingu, vyahaki kutoangaza
Napia nazovurugu, ujingani ng'ang'aniza
Litimize lengo lake, babu yangu abdullah

Tunamuombea Dua, afuu makosa yake
Juhudi zake pokea, zidisha malipo yake
Yalomema mpatia, Leo nayokesho yake
Litimize lengo lake, babu yangu abdullah

Tulinde kizazi chake, mtini tusije shuka
Tuzifwate nyayo zake, imara dini kushika
Zikubali Dua zake,utujalie baraka
Litimize lengo lake, babu yangu abdullah

Mtunzi
Masihi omary stambuli kisagwa

IWE KWA RADHI ZA MUNGU

Kwa Jina Lako ambalo, huzitetemesha mbingu
Sikiza nikuombalo, Unijibu Mola wangu
Nipe nilitamanilo, Uwe radhi nami Mungu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Kila jambo nifanyalo, Iiwe kwa radhi za Mungu,
Kubwa lishangaliwalo, kisivimbe kichwa changu
Nalidharauliwalo, nisijali malimwengu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Lije lihangaishalo, utulie moyo wangu
Jeusi liogopwalo, lifanye si kitu kwangu
Liwe zuri lipendwalo, yasilale macho yangu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Lile nilidhanialo, ndani lina kheri yangu
Ila Allah Ujualo, halina maana kwangu
Fanya niridhike nalo, lile upendalo Mungu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Lolote nilikosalo, ushukuru moyo wangu
Iwe kunywa au mlo, ladha yangu uwe Mungu
Gawio nilipatalo, nisifu Mpaji wangu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo

Lolote niliwazalo, ipe nuru roho yangu
Na lile nijifunzalo, lipambe ubongo wangu
Kila lengo nishikalo, liwe la kuumbwa kwangu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo

Neno nikaribialo, kunena ulimi wangu
Kabla kutoa hilo, zipime mizani zangu
Ni kao gani liwalo, itanihesabu mbingu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo

Nikwepe lipofushalo, la mafungamano yangu
Nichunge niambiwalo, toka maswahibu zangu
Nishike jema ambalo, kanena adui kwangu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Tendo niliambatalo, nikhalisi nia yangu
Lile nilipatialo, izidi hofu ya Mungu
Na lile nikosealo, nitubu unyonge wangu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Jambo nilaumiwalo, madamu haki ya Mungu
Liweje nidhaniwalo, litiwe kizunguzungu
Wacha naliwe liwalo, nisijali hadhi yangu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Liwe lifedheheshalo, liso la heshima kwangu
Lakini litukuzalo, Jalali ya Mola wangu
Mie niambate hilo, nikiyameza machungu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Nalivume livumalo, nijishushe ndani yangu
Liwe utapiamlo, au kichaa wa Mungu,
Nipuuze lisemwalo, isiyumbe nia yangu
Iwe kwa radhi za Mungu, kila jambo nifanyalo.

Kosa nikosolewalo, isinyonge dhati yangu
Na safi nisifiwalo, isife dhamira yangu
Mwisho unipe malalo, yafiche mzoga wangu
Kila jambo nifanyalo, liwe kwa radhi za Mungu.

Vuno la ujinga wangu, Mola unikinge nalo
Lisiwepo tendo langu, shetani aliibalo
Zipotee nguvu zangu, kisa nijione kwalo
Kila jambo nifanyalo, liwe kwa radhi za Mungu.

Sh. Ame

SIJAFA SIJACHELEWA-NINAKUOMBA JALALI

Pekee nikuombae, ni Weye Mola Jalia
Nimekwama nikwamue, Dunia inavutia
Nifanye niikatae, ijapo inanukia
Sijafa sijachelewa, ninakuomba Jalali

Ina nguvu na sifae, kutughilibu nsia
Kwa vishawishi hadae, usoni kutuletea
Si wa ibada asee, tumeipotea njia
Sijafa sijachelewa, ninakuomba Jalali

Ni mumo nisikatae, shetani kunipitia
Ni mengi anijazie, niaye kunipotoa
Asema nifurahie, kumbe ya kuangamia!
Sijafa sijachelewa, ninakuomba Jalali

Miye huyo huyo mie, Mola wangu itikia
Dhambi zangu Nifutie, dhambi nisije rudia
Naomba Nighufirie, kwako ninanyenyekea
Sijafa sijachelewa, ninakuomba Jalali

Ninatamani nilie, ole wangu kujutia
Na machozi niyatoe, kimya kimya nikilio
Na chini nigaegae, natubu nilokosea
Sijafa sijachelewa, ninakuomba Jalali

Al-Ustadh Mhenga
Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile Mbagala Rangitatu
Dar es Salaam

Mwanga

Kiza sisawa na mwanga, japo cheche iwapo
Hata Cha Kuni kijinga,takufikisha pawapo
Gizani utajifunga, usijue uwendapo
Uutafute ulipo, utambue uendako

Mwanga ndiyo hasa Nuru, hung'aa nakuangaza
Hukufanya uwe huru, kufikiri nakuwaza
Kuiepuka kufuru, haki kujing'ang'aniza
Uutafute ulipo, utambue uendako

Mwenye Nuru anang'aa, mwanga hupata eneza
Aoneka kama taa, kiza akikifukuza
Vyakaribu tavijua, mwanga uloviangaza
Uutafute ulipo, utambue uendako


Haufichiki mwangaza, utaoneka ulipo
Jitihada ongeza, tusikusake uwapo
Mdomo utanyamaza, Nuru Yako itawepo
Uutafute ulipo, utambue uendako

Masihi Omary stambuli kisagwa

KULISHA

Halishwi yeye hulisha, Rabbi mtoa riziki
Sifa hino inatisha, nani anaimiliki?
Nani aweza kuvisha, lau lapa la kaniki?
Udongo walima pamba, nani kautengeneza?

Na Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba Kiwalani - Dar es salaam.



Mbweha na zabibu

Mtandaoni



Kulikuwa na mbweha mwenye njaa na kiu msituni. Kitu maskini alikuwa kutafuta mawindo kwa masaa, bila kuwa na bahati yoyote.



Baada ya kutumia siku nzima kutangatanga msituni, aliweza kuona nguzo ya zabibu tamu, ambayo ilining'inia kutoka kwa mzabibu mrefu.

Mbweha, akiwa amekata tamaa, alitaka kuwafikia. Aliruka na kuruka, lakini hakuweza kufika kwao. Baada ya majaribio mengi, mbweha alichoka.




Bah, sijali tena. Jumla, kwa nini nataka kula zabibu hizo? Wana hakika kuwa kijani na mwamba mgumu! Acha mtu mwingine ale ... '

Na baada ya kusadikika kwake, **aliondoka akijiamini anastahili sana kutoa tunda lililokuwa likingojewa kwa muda mrefu**.

Maadili:

ikiwa jambo fulani haliwezi kufikiwa au linaonekana kuwa haliwezekani, usilaumu wengine au mazingira. Kila moja ina uwezo wake na, pia, mapungufu.

Unganisha Nukta



MAPISHI YA NDIZI MZUZU (MBIVU)ZA NAZI

Mara nyingi tunakula ndizi mzuzu za kuchemsha, ukijaribu mapishi haya unaweza usile tena mapishi ya kawaida ya ndizi mzuzu. Utamu wake ni wa kipekee na hiki ni chakula bora, na hakina vikorombwezo vingi.

Mahitaji,
Nazi 1,
Ndizi mzuzu zilivoiva 6,
Sukari kijiko 1 cha chai na
Iliki.



Maelekezo

Menya ndizi na zikate kwa urefu ili utoe ule uzi mweusi katika kiini cha ndizi. Usitupe maganda. Menya hiliki na kisha zitwange
Kuna nazi na uchuje tui zito na jepesi.

Katika sufuria ya kupikia, panga maganda ya ndizi mzuzu,vizuri na kisha juu yake panga ndizi vizuri.

Bandika sufuria jikoni na kisha weka tui jepesi.
Acha kwenye moto ichemke hadi tui likauke.

Weka sukari kidogo kwenye ndizi na weka Iliki.
Weka tui zito kisha ache lichemke kwa moto mdogo sana hadi tui likauke.
Unaweza kuepua na kujilamba.

TUSIYOYAJUA KUHUSU QUR'AN TUKUFU
KUHIFADHIWA KWAKE

Kutoka Uk> 05

pamoja na wale maswahaba wanne ambao Mtume Muhammad[saw] alikuwa akiwasomesha Qur'an Tukufu nzima walikuwepo wengine ambao walikuwa wakijifunza kwake sehemu sehemu za Qur'an Tukufu sawa na kauli ya Hadharat Umar (r.a) ya kwamba alikuwa amefundishwa kutamka neno fulani kwa njia maalumu yaonesha kwamba yeye naye alikuwa akijifunza sehemu za Qur'an Tukufu kutoka kwa Mtume Muhammad[saw] mwenyewe.

Ile tofauti iliyotokea baina ya Hadharat Umar (r.a) na Hadharat Abdullah bin Masuud (r.a) haikuhusika na mageuzi yoyote ya maneno ya Qur'an Tukufu hii ilihusika na irabu moja hali ya kuafikiana na baadhi ya irabu ni sifa ya pekee ya lugha ya kiarabu na kuhusu vitenzi fulani kubadilishana irabu kwa irabu nyingine kunaruhusiwa wala hakuathiri maana mathalani wakati mwingine herufi yenye kupindua ulimi au kama mazoea ya kikabila au kifamilia lakini kati ya hali hizo zote mbili maana ya kitenzi chenyewe inabakia palepale kwa kufahamu mbinu hizi za kilugha Mtume Mtukufu Muhammad[saw]kwa maelekezo ya kiungu akatoa ruhusa yatumike matamshi haya kwa kuwa kutumika hivyo hakukuwa na athari mbaya ya kubadili maana au tafsiri za maneno kwa kuwa watu wasioongea lugha ya kiarabu sifa hii ya kipekee ya lugha ya kiarabu hawakuizoea basi wao huelekea kujiwa na hii dhana ya kimakosa kwamba matamshi hayo ya hivi na vile yanamaanisha mabadiliko katika matini ya Qur'an Tukufu na kwamba Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa na mazoea ya kumsomesha mtu mmoja aya fulani za Qur'an Tukufu kwa njia moja na mwingine kumsomesha kwa njia nyingine kusema kweli hakikufanyika kitu cha aina hiyo hizi tofauti ambazo zimekuja kuwa jambo la kuzungumziwa hazikuwa ni tofauti za mageuzo ya maneno ya Qur'ani Tukufu wala hayakuwa mageuzi ya neno. Zote zilihusika na matamshi ya irabu ambayo hayakubadilisha kivyovyote vile maana au uzito wa neno, tofauti ya pekee ilikuwa kwamba baadhi ya makabila au familia kwa kuzoea kwao kutamka vitenzi fulani kwa vina mahususi na kwa njia fulani waliruhusiwa kufanya hivyo.

QUR'AN TUKUFU YAHIFADHIWA KWA MOYO

Kusemakweliyafahamikakwamba idadi kubwa ya masahaba wa Mtume Muhammad[saw] walikuwa wakiijua Qur'an Tukufu nzima kwa moyo kama ilivyosimuliwa hapo awali katika kurasa za mwanzo. Kuhusiana na kile kisa cha sehemu iitwayo Bir Mauna kwenye mwaka wa 4 Hijiria Mtume Muhammad (s.a.w) aliyatumia makabila fulani masahaba zake 70 wakawe wakufunzi na kila mmoja wao aliijua kwa moyo Qur'an Tukufu wale waliokuwa wakiijua Qur'an Tukufu nzima kwa moyo walipitisha sehemu kubwa ya wakati wao wakiwasomea wengine saa zote za mchana na usiku. Hadhrat Abuu Yala anasimulia kwamba safari moja Mtume Muhammad[saw] aliambiwa kwamba Hadhrat Abuu Musa (r.a) alikuwa akiwafundisha watu usomaji wa Qur'an Tukufu katika nyumba yake.

Mtume Muhammad[saw] akataka apelekwe mahali ndani ya nyumba ile ili aweze kumsikiliza Hadhrat Abuu Musa bila kujulikana na wale waliokuwepo basi akapelekwa mahali kama hapo kule nyumbani na baada ya kumsikiliza Hadhrat Abuu Musa akiwa anaisoma Qur'an Tukufu Mtume Muhammad [saw] akaridhia usomaji wake na ukamfurahisha mno na akatamka akisema 'unasoma Qur'an Tukufu kwa ule mtindo wa kuvutia wa Nabii Dawud[as] '{muslim kitaabus-salaat}.

Kisa hiki chaonyesha kwamba Mtume Muhammad (s.a.w) alifanya juhudi kusimamia usomaji wa Qur'an Tukufu wa watu minghairi ya wale wanne aliokuwa amewateua kama wakufunzi wakuu wa Qur'an Tukufu na alitaka sana kuona kwamba haliingii kosa lolote katika usomaji wao.

Hadhrat Imam Ahmad bin Hambal anasimulia kufuatana na kauli ya bwana Jabir bin Abdullah ya kuwa safari moja Mtume Muhammad[saw] alipofika msikitini aliwakuta watu wakisoma Qur'an Tukufu na akatamka akisema someni vizuri na jitahidini kujipatia radhi ya Mwenyezi Mungu kwa njia hiyo kabla haujaja wakati ambapo watu wataisoma sawasawa lakini kwa lengo la kuifanya kuwa ni kiwezesho cha kujichumia riziki zao badala ya kuwa ni kiwezesho cha kujitakasa nyoyo zao.

Hadhrat Jabir bin Abdullah anasimulia kwamba wale waliokuwa wakiisoma Qur'an Tukufu katika kisa hiki hawakuwemo Muhajirin na Ansar tu bali pia wakazi wa jangwani na wasiokuwa waarabu.

Kwa mwendelezo wa Makala hii piga simu au WhatsApp +255 658 971 662

MATUKIO KATIKA PICHA



Mhe. Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania alikuwa mgeni rasmi, katika mkutano mkuu wa mwaka Mkoani Pwani. Viongozi mbali mbali pia walishiriki mkutano huo. Pia wanajumuiya walitoa unit 18 za damu kwa idara ya damu salama.



Amir Sahib jamaat Ahmadiyya Tanzania alionana na MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Tar. 14 Januari 2025 Dares Salaam.



Sh Abid Mahmood bhatti Sahib (Naibu Amir) alishiriki na kuongoza Dua katika madhimisho ya siku ya sheria katika Mahakama kuu ya kanda ya Morogoro.



Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib (Naibu Amir) na na Sheikh Karimuddin Shams Sahib (Sheikh Dodoma), walipata mualiko katika mkutano wa uzinduzi wa sera ya elimu na mafunzo chini ya wizara ya elimu, sayansi na technologia mjini Dodoma.

Maswali kutoka katika kitabu cha

MHISANI KWA UBINADAMU

Imetayarishwa na.
Sheikh Ali Dino Tahir - Simiyu

Uk. 65,66

89. Ni wakati gani waislamu wanaruhusiwa kumbadili mtu huru kuwa mtumwa?

Jb. Ikitokea vita vya dini na watu wakiuwawa katika vita ile na wengine wakikamatwa baada ya ushindi ,sasa waliokamatwa wale tu watahesabiwa kuwa ni watumwa.

90. Dini iliyoletwa na Mtume Muhammad saw ,je inaruhusu kumfanya mtumwa aliye huru bila ya vita

Jb. Hapana,Muislamu Atakayemnyima uhuru mtu yeyote na kumfanya awe mtumwa atafahamika kama amemuua.

91. Mtume Muhamad SAW alisemaje kuhusu kuishi na watumwa

Jb. Mtume Muhammad saw alituamru kwamba tuwaite watumwa wetu "Ndugu" sio mtumwa au mhudumu,wakikwama katika kazi tuwasaidie,tukiwapa kazi ngumu tufanye nao hiyo kazi pamoja,tuwape chakula tukilacho,tuwavishe kama vile tukivaacho na ikitokea safari wapande na usafiri kama sisi, tukiwapiga kwa sababu ya kosa fulani basi tuwaache huru,wakitaka kufunga mikataba kwa ajili ya uhuru wao waachwe huru ili wafanye vibarua sehemu fulani wakalipe fidia yao ili wapte uhuru kikamilifu na baada ya vita ya uhudi Mtume SAW alisema watumwa wakisomesha waislamu kumi kusoma na kuandika basi waachwe huru.

Uk. 67

92.Kwanini baadhi ya watumwa hawakutaka waishi huru hali walipewa uhuru?

Jibu: Waislamu waliambiwa masharti yaliyorahisisha sana Maisha ya watumwa kwa sababu waislamu walikuwa wanawalea kama ndugu zao wa karibu badhi ya watumwa waliona wakianzisha Maisha yao hawatoweza majukumu, ni bora wakae kama watumwa na wafaidike.

Uk. 68, 93. Utbah ambaye aliyekuwa ni kiongozi mkubwa alipotumwa na wakuu wa Makka ili amshawishi Muhammad saw aache kutangaza umoja wa Mungu badala yake watampa atakavyo , Mtume Muhammad saw hakukubali kabisa na alimsomea baadhi za aya za Quran ambazo zilimuathiri Utbah. Aliporudi aliwaambia nini wakuu wa Makka?

Jibu: Aliwaambia kuwa huyu si muongo wala si mchawi,acheni kumpinga.

Uk. 69, 94. Hisani za Mtume zilikuwa za aina gani ?

Jibu: Hisani za Mtume hazikuwa za muda mfupi,bali zilikuwa ni za kudumu na za viwango vya juu kama vile mama afanyavyo hisani kwa watoto wake.

Uk. 70

95. Watu wakiwa na Imani kwamba vitu vilivyopo duniani ni miungu,watapata hasara gani ?

Jibu: Watu hawatatafakari kamwe kuhusiana na faida zao za asili.

Uk. 71

96. Watu wakiwa na Imani kwamba Mwenyezi Mungu aliviumba vitu vyote kwa ajili ya manufaa yao , watapata faida gani ?

Jibu: Watu wakiwa na Imani kwamba vitu vyote vimeumbwa kwa faida yetu basi watajaribu kwa kila namna ili wajue faida za vitu vile na kuapata maendeleo.

Uk. 72 97. Wakati wa Mtume SAW watu wangapi walikuwa wakijua kusoma na kuandika katika mji wa Makka?

Jibu: Watu saba tu.

98. Toa Tafsiri ya Hadithi hii ya Mtume SAW "Twalabul ilmi faridhatun ala kulli muslimin wa muslimatin"

Jibu: Kutafuta elimu ni faradhi kwa kila muilamu mwanaume na mwanamke.

Uk. 73 98. Sawa na agizo la Mtume SAW kuhusu kupata elimu waislamu walivumbua elimu mbali mbali na kupata maendeleo makubwa katika sayansi wakati ule wanazuoni wakristo walikuwa wanasemaje kuhusu kujielimisha?

Jibu: Wakati huo wanazuoni wa kikristo walikuwa wakisema kuwa ni kufuru kujielimisha.

99. Mwandishi wa kizungu aliandika nini kuhusu huduma za waislamu katika Hispania.

Jibu: Mwandishi wa kizungu anakiri kwamba kama elimu isingefika Uhispania kwa njia ya Waislamu basi sisi leo tungekuwa katika ujahili wa kiwango cha juu sana.

100. Karne chache baada ya kufariki kwa Mtume Muhammad SAW nasaha zake upande wa elimu zilifanya kazi gani?

Jibu: Kwa sababu ya mafundisho ya Mtume Muhammad SAW maendeleo ya kielimu yakaendelea kwa mfululizo

Uk. 74 101- . Sawa na Mafundisho ya Mtume SAW ,je Elimu kina kikomo na mwisho

Jibu: Elimu haina mwisho ,hivyo tumesisitizwa na Mtume SAW kwamba dumuni kufanya utafiti muda wote wala msigote

102. Kuna dalili gani kwamba elimu haina mwisho

Jibu: Mwenyezi Mungu ndiye alikuwa anamfundisha Mtume Muhammad SAW kila kitu na yeye alikuwa ajuaye kuliko sisi wote, naye aliagizwa na Mungu kwamba aendelee kuomba رب زدنی علما RABBI ZIDNI ELIMA yaani Ewe Mola wangu izidishe elimu yangu,hii inamaanisha elimu haina mipaka.

103. Mtoto anapoanza shule waislamu wanapaswa kumhifadhisha dua gani ili adumu kumuomba Mungu

Jibu: رب زدنی علما RABBI ZIDNI ELIMA yaani E, Mola wangu izidishe elimu yangu

Uk. 75 104 . Je, kuna maradhi au ugonjwa ambao hauna tiba.?

Jibu: Hapana, Mtume SAW alisema kwamba لکل داء دواء LIKULLI DAAIN DAWAA yaani "Mwenyezi Mungu ameandaa tiba ya kila maradhi" ,kwa hiyo tusikate tamaa na tusikubali wagonjwa wafe bali tuwatafutie dawa.

Uk. 76 105. Mtu akiwa mchafu kitabia na mbaya sana je, anaweza kuwa mtu mwema,akitubu.?

Jibu: Bila shaka ataweza kuwa mwema akitubu na kutokurudia mambo yake maovu,kikubwa asikate tamaa na Mwenyezi Mungu

Uk. 77 106. Toa Tafsiri ya Sura Yusuf aya 88 انہ لا یا یئس من روح اللہ الا القوم الکافرون INNAHU LA YAYIASU MIRROHILLAHI ILLAL KAUMUL KAFIRUUN

Jibu: Hakuna yeyote akataye tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu ila wale wenye kukataa (amri zake)

107. Mtu aliyefanya maovu mengi ,akiamini kwamba hatosamehewa kamwe,kuna hasara gani katika hilo

Jibu: Akiamini hatosamehewa atazidi kufanya maovu mengi lakini akiamini anaweza kusamehewa ataacha muda wowote ule ,anaweza kuwa mtu mwema kabisa.

108. Uzitaje hisani sita za Mtume Muhammad SAW zilizoandikwa katika kitabu kuazia ukurasa 70 hadi 77 ?

Jibu: 1. Kuondoa shirki 2.kutufahamisha kwamba sayansi haipingani na dini ya Islam

3. kutubainishia kwamba elimu haina mipaka wala mwisho 4.Kutuambia kwamba kila ugonjwa una tiba yake.

5. Alitufahmisha kwamba tusikate tamaa,Mungu anaweza kutusamehe dhambi zetu, tukitubu

109. Kamilisha sentensi : Mtume Muhammad SAW alitoa fundisho kwamba "Jitihada ya kweli huwa…….?

Jibu: Jitihada ya kweli huwa asilan haipotei bure.

Uk. 78 110. Je, Dua au maombi ya Masingasinga,Wahindu au Wakristo yanakubaliwa?

Jibu: Bila shaka kwa jili ya utafutaji wa muongozo dua ya kila mtu hukubaliwa.

111. Uieleze Hisani ya sita ya Mtume SAW iliyoandikwa katika kitabu cha Mhisani kwa Ubinadamu?

Jibu: Alistawisha usawa wa kibinadamu baada ya kufutilia mbali matabaka tabaka baina ya watu.

Uk. 79,80 112.Fadhila na ubora wa mtu unatokana na nasabu yake au kabila lake au ukoo wake?

Jibu: Fadhila na ubora wa mtu unatokana na ucha Mungu wake au takwa yake tu

Uk. 81 113.Kitabu cha mayahudi kinawafundisha nini kuhusu kuchukua riba kwa watu?

Jibu: kumbukumbu 23:19 inasema : "Usimkopeshe ndugu yako kwa riba …mgeni waweza kukopesha kwa riba" katika hukumu hii Torati imependelea watu wake lakini Quran tukufu inazuia kabisa kukopesha kwa riba na mtu yeyote.Anayechukua riba ,anafunga vita na Mungu (Sura Albakara aya 280)

Uk. 81,82 114.Mtume Muhammad SAW alisema انصر اخاک ظالما او مظلوما UNSUR AKHAKA DHALIMAN AU MADHLUMA yaani Enyi waislamu msaidieni ndugu yenu hata kama awe ni mdhalimu au mdhulumiwa ,Mtume alipoulizwa kwamba mdhalimu tutamsaidiaje, alijibu nini ?

Jibu: Mtume alijibu kwamba Msaidieni mdhalimu kwa kumzuia ili asiweze kudhulumu.

Uk. 83 115. Mtume Muhammad SAW alipokuwa anaenda katika vita ya uhudi ;watu wawili waliotoka Makka walikutana naye na kusema wanataka kusilimu na kushiriki katika vita na walimuambia lakini walipotoka Makka waliwaambia makafiri kwamba hawatosaidia waislamu. Mtume aliposikia aliwaambia nini?

Jibu:Mtume SAW aliwaambia kwamba msishiriki katika vita,itakuwa ni uvunjaji wa ahadi.

Uk. 84 116. Kamilisha sentensi ifuatayo : Yeyote yule aliye duni au aliyetukuka,wote……

Jibu: Yeyote yule aliye duni au aliyetukuka, wote wako sawa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Uk. 85 117.Mapigano mengi husababishwa na nini?

Jibu: Mapigano mengi husababishwa na Imani ya kwamba mbali nasi dini za wengine ni za uongo,Mtume SAW alifuta wazo hilo.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Walimu na Masheikh waliohudumu Zanzibar

Kutoka uk. 12

Mbanga zilipatikana BAIAT kadha, zilizodumu ni nne (4). Baada ya mwalimu Mbanga kupewa uhamisho Mwl Said Othman aliendelea kuhudumu kwa njia ya kujitolea hadi mwaka 2013 na Baiat 12 zilipatikana.

2. Mwalimu wa pili kutumwa Zanzibar ni Mwalimu Mussa Omar Budi yeye alihudumu tokea mwaka 2013 hadi mwaka 2018. Katika kipindi hiki Baiat zilizodumu ni tisa (9) ni katika kipindi hichi ambacho Jamat mbili zilizaliwa Maungani na Unguja Ukuu na kuifanya Zanzibar kuwa na jumla ya Jamati tatu. Migombani, Maungani na Unguja Ukuu.

3. Wa tatu kutumwa Zanzibar ni Sheikh Mussa Issa mwaka 2018 hadi 2019. Jumla ya baiat zilizodumu kwa kipindi hiki ni tisa (9)

4. Wa nne ni Sheikh Hussein Yussuf Ngamilo mwaka 2019 alihudumu hadi mwaka 2022. Tunazo baiat nne za kipindi hiki .

5. Wa tano Mwl Muhyidin Mfaume Gamba ambaye aliripoti tarehe 25 Disemba 2022 anaendelea mpaka makala hii inaandikwa.

MALI ZA JUMUIYA NA UJENZI WA MISIKITI

Mnamo mwaka 2013 Jumuiya ilinunua eneo Maungani. Mwaka huo huo Wanajamat walijenga nyumba ya mwalimu (Mission house) na madarasa mawili kwa ajili ya kusalia na kufundishia watoto. Na mwaka huo huo alitumwa Mwalimu Mussa Omar kwa ajili ya huduma za Kiofisi.

Wanajumuiya walielekeza nguvu zao kwenye ujenzi wa Msikiti .Kwa sababu kadha wa kadha ujenzi wa msikiti ulichelewa hadi mwaka 2022. Msikiti wa Maungani ulifunguliwa na Amiri na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry siku ya tarehe 15/06/2024 sawa na mwezi 8 Mfungu tatu 1445 Hijiria. Jina la Msikiti ni "BAITUL- AWWAL" JAMAAT YA UNGUJA UKUU

Historia ya Ahmadiya Jamati ya Unguja Ukuu ilianza mwaka 2009 ambapo mwanajumuiya kutoka Tanzania bara Bw Salum Mikidadi alikuwepo huko Unguja Ukuu kwa shughuli binafsi alifanya mahubiri ya kimya kimya . Bw. Salum Mikidadi alifikisha ujumbe kwa Bwana Mohd Mzee na wenzake wachache kutokea mwaka huo 2009.

Baada ya kujiridhisha bwana Mohd Mzee ambaye ndiye alikuwa imamu wa hapo aliamua kumpokea imamu wa zama akajaza Biat mwaka 2013 akawa Ahmadiya wa kwanza Unguja Ukuu. Wapili ni mwanawe Maalim Mzee Mohd na wengine wakafuata kadiri siku zilivyopita Bwana Mohd Mzee ndiye rais wa tawi la Unguja Ukuu. Mwaka 2017 walijenga msikiti mdogo wa tope ambapo walianza kusali ljumaa kwani hapo kabla iliwalazimu kusali ljumaa Maungani umbali wa kilomita 20.

Bwana Mohd Mzee ameshatoa ardhi yake wakfu kwa ajili ya kujenga msikiti . Ujenzi wa msikiti wa matofali umeanza mwaka 2023 na unaendelea vizuri. Tawi la Unguja Ukuu pamoja na wanajamati wachanga kuna wanajumuiya wa zamani kama vile Bw Ameir Mahmoud Kheri na Bi Amina binti Mohd nao wanaishi huko baada ya Tawi kupatikana.

Maendeleo haya ni kwa msaada mkubwa wa Allah kwani haikuwa rahisi wala si kwa ujanja wetu. Masheikh wa Zanzibar walishaapa kwamba Ahmadiya haitaingia Zanzibar asilani abadani.

MSAADA WAKE ALLAH (S W)

Kuingia Ahamdiya Zanzibar ni uthibitisho tosha kwamba Ahamdiya ni jumuiya yake Allah vinginevyo isingefanikiwa. Mimi mwandishi wa makala hii ni shahidi juu uadui wa Masheikh wa Zanzibar dhidi ya Ahmadiya, niliwekwa mahabusu kituo cha polisi Malindi eti kwa kosa la kuuza vitabu vya Kiahmadiya bila ya leseni ya biashara. Pemba pia niliwekwa mahabusu kituo cha polisi Mkoani kwa amri ya Sheikh tu.

Mwaka 2007 alipojiunga Hayati Fatma Hassan Ali ilikuwa uhasama mkubwa sana . Fatma alifikishwa kwa mkuu wa Wilaya na mahakamani kwa kosa la kuingia katika Ahmadiya Ikasemwa ameritadi. Miongoni mwa waliofikishwa mahakamani ni Bw Mohd Othman Khatib na Bw Abdul-azizi Juma Kindy. Kuna baadhi ya walioacha Ahmadiya kutokana na vikwazo walivyoekewa hususan kwenye ndoa zao kwa kuambiwa kwamba chagua moja ama uache Ahamdiya ubaki na mwenetu au umwache mwenetu ubaki na Ahmadiya yako . Wako walioacha Ahmadiya kwa sababu ya vikwazo kama hivyo na hila nyengine nyingi. Hayati Bw Shaib Kondo alikatazwa kuswali kwenye msikiti fulani jirani na nyumbani kwake kisa ni Ahmadiya.

KISA CHA SHEIKH MBONGO

Siku moja miongoni mwa masiku mtangazaji alitutangazia wanakijiji cha Ukutini Pemba kwamba yupo Sheikh kutoka bara ambaye kesho tukijaaliwa atatoa waadhi msikitini. hivyo munatakiwamufike msikitini nyote wake kwa waume wakati wa adhuhuri.

Tulivyoamka mimi sikuwa na azma yakwenda kumsikiliza Sheikh. Nilikwenda shambani kwangu, karibu na wakati wa adhuhuri nilihisi unyong'onyevu fulani kwa hiyo nikaamua kurudi nyumbani .Nilipofika nyumbani baada ya kuswali nilitamani niende nikamsikilize Sheikh huyo wa Bongo.

Msikiti ulikuwepo jirani tu sio mbali , nilifika msikitini nikakaa nje barazani. Sheikh wa Bongo alikuwa amesimama anaendelea na mawaidha na msikitini watu wamejaa wanamsikiliza. Haukupita muda mrefu nikamsikia Sheikh anamtaja Masihi aliyeahidiwa akisema kwamba alijidaiya utume wa uongo. Nilijisikia kama kwamba nimepata shoti ya umeme mwili ulisisimka kwa sababu ya maneno hayo ya sheikh wa Bongo. Nilitamani nione sura yake nikataka kuingia msikitini ila nilikosa nafasi nikabaki kizingitini, hata hivyo niliweza kumuona sheikh, alipomaliza hutuba yake alikaa chini na kukaribisha maswali. Nilikuwa wa kwanza kunyanyua mkono wangu, alipouona mkono wangu akasema ehe uliza. Nilisimama huku nikijitahidi kutuliza ghadhabu zangu na kwa upole nilianza kwa kumshukuru Allah na kumpongeza sheikh kwa ujio wake.

Nilimwambia kwamba kazi ya daawa ni nenye manufaa sana ndani ya uislamu na ina thawabu nyingi kwa waifanyao.

Baada ya hapo nilimgeuzia kibao kwa kusema ila mimi nimehuzunika na kitendo cha kumkashifu hadharani kiongozi wa dini Mirza Ghulam Ahmad (a.s) na kumuita yeye muongo. Basi nakuomba uthibitishe uongo wake na mimi ambaye nimemwamini nithibitishe ukweli wake. Baada ya kusema hivyo nikasubiri jawabu sheikh alisimama kwa shida huku akitetemeka na wenyeji wake waliokaa karibu naye wakimsihi akae, kwa shida aliweza kutamka" kama unataka hivyo twende kwenye televisheni" mimi nikamjibu. Niko tayari. Akasema

"na Masheikh wa Sudan wawepo" nikajibu tayari wawepo Wasudani hata wa Saudia . Muda wote huo wenyeji wake walikuwa wakimvuta kanzu ili akae chini.

Hatimaye sheikh alikaa chini ikapigwa fat-ha ikasomwa dua ya kufungia kikao na mkutano ukaisha hivyo. Tulipotoka msikitini sheikh Swaleh Omar Kaabi alinisogelea akanambia maneno haya yafuatayo:-

" Usiwe na wasiwasi sheikh Ali , Allah atamdhalilisha yeyote atakaejaribu kudhalilisha Uislamu, mimi niliitikia amin. Na huyu sheikh Kaabi na ukoo wake wanajuilikana kuwa wao ni masharifu wanaosadikiwa kwamba dua zao zinakubaliwa sana.

Itaendelea toleo lijalo in shaa Allah

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenziya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah

UK. 03






Buriani Salum Dadi Mtamila

Uk.03

Walimu na Masheikh waliohudumu Zanzibar

Na. Ali Hamisi Juma Sahib



Kabla ya markazi kutuma mwalimu Zanzibar Maalim Said Othman alihudumu kwa njia ya kujitolea yeye ni mwanajumuiya aliyepata mafunzo rasmi katika chuo cha Jamia Morogoro.

1. Mwalimu wa kwanza kutumwa Zanzibar ni Mwl Abdalla Khamis Mbanga. Alitumwa mnamo mwaka 1993 na alihudumu hadi mwaka 1996 chini ya Amir Sheikh Bajwa . Mwl Mbanga Ameelezea kwamba wakati huo sheikh aliyekuwa akiwika Zanzibar ni Sheikh Nassor Bachu, Mwl Mbanga anaelezea kwamba siku moja Sheikh Nassor Bachu alitoa hutuba kuhusu majinni yeye mwl Mbanga akaiita hotuba hii kuja kushindana katika hoja na Sheikh Nassor Bachu kwa njia ya sauti (audio). Sheikh Bachu aliomba mjadala na Mwl Mbanga alikubali lakini siku ya mjadala ilipofika Sheikh Nassor Bachu hakuhudhuria. Mjadala haukufanyika. Hii ndio Ahmadiya bwana. Kila ajae mbele anapigwa.

Bakathiri alipigwa, Farsy alipigwa na Bachu kadhalika. Katika kipindi hichi cha Mwl



HABARI UK> 11

JALSA SALANA QADIAN KIINI CHA SAFARI YA KIROHO

Na Yassin Saleh
Dhamin(M.A.History-University of DSM


UTANGULIZI

Hapana shaka yeyote, Jalsa Salana Qadian ina taadhima na nafasi ya kipekee katika nyoyo



za waahmadiyya duniani kote. Qadian inatoa taswira yenye mng'ao wenye shani kuhusu Islam kama inavyofafanuliwa na kuwekwa bayana na

UK. 03





Je, Wajua?

Jonny Kim ni Luteni Kamanda wa Jeshi la Wanamaji la Marekani, aliyekuwa Navy SEAL, daktari (M.D. kutoka Shule ya Matibabu ya Harvard), naval aviator, na astronaut wa NASA.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 2,800/=.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com